

Kamati ya Shule ni Nini?

Kamati ya shule ni nini?

Kamati ya shule ni kikundi cha wajumbe waliochaguliwa kwa ajili ya kuongoza na kuangalia shughuli za shule ya msingi kwa msaada wa jamii. Kila shule ya msingi kisheria inatakiwa kuwa na kamati ya shule. Kamati ya shule ina dhima ya msingi katika kutekeleza Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM)

Nani ni wajumbe wa kamati ya shule?

MMEM inakusudia kuongeza demokrasia, ushiriki na uwajibikaji katika muundo na kazi za kamati ya shule. Nakala ya MMEM haijaonyesha wazi wajumbe wa kamati ya shule ni akina nani, lakini inasisitiza wawakilishi kutoka katika jamii, walimu, wanafunzi, wazazi na serikali ya kijiji. Pia inahimiza usawa wa kijinsia ili kuhakikisha sauti za wasichana na wanawake zinasikika.

Kamati ya shule ina majukumu gani?

Kamati ya shule inahusika na masuala yote ya shule kwa ujumla. Kwa mujibu wa kiambatanisho cha MMEM majukumu yake makuu ni:

- Kuhamasiha, kuhusisha na kuwasilisha habari za elimu kwa wazazi wote, wanafunzi,wadau katika jamii na watendaji na mamlaka ya serikali za Mtaa/Kijiji.
- Kushughulikia masuala ya shule ya kila siku, pamoja na utekelezaji wa vipengele vyote vinne vya MMEM.
- Kushirikiana na mwalimu mkuu na walimu wengine kuweka vipaumbele na kuandaa Bajeti na Mipango ya Maendeleo ya shule.
- Kufungua akaunti na kusimamia kwa uhakika na uangalifu fedha zilizo pokelewa kwa ajili ya utekelezaji, kuhakikisha uwajibikaji wa hali ya juu na uwazi katika mchakato unaotumika, ikiwa ni pamoja na kuweka wazi mapato na matumizi kwa jamii.
- Kuandaa na kutoa kwa usahihi na kwa wakati mwenendo na ripoti ya fedha kwa jamii, Kata na Halmashauri.

Hii inamaanisha kwamba kamati ya shule imepewa mamlaka ya kuunganisha jamii kuakisi changamoto zinazojitokeza kuhusu ubora wa elimu kwa wote na kutafuta suluhisho yakinifu ndani ya miongozo ya Serikali. Hawatakiwi kuendelea kusubiri kupokea maelekezo ya kila kitu kutoka ngazi ya juu. Serikali itasaidia kamati za shule kifedha na miongozo ya sera kwa ujumla, lakini ni jukumu la wananchi kuzitumia na kuboresha elimu katika jumuiya yao.

Kamati ya shule inawajibika kwa nani?

Kamati ya shule inatakiwa kuwajibika kwa wadau wake: wanafunzi, wazazi, walimu na jamii inayoizunguka shule. Hii ndio sababu taarifa, mrejesho na uwazi ni muhimu katika ngazi ya jamii na pia ni sababu kwa nini kamati ya shule itunze kumbukumbu nzuri. Katika hotuba yake ya Septemba 2002 kuhusu MMEM, Rais Mkapa alisisitiza:



> " Ili kuimarisha demokrasia , kila shule inatakiwa kutoa taarifa ya mapato na matumizi katika Serikali ya Kijiji/Mtaa kila miezi mitatu katika kikao cha Halmashauri. Sambamba na kutoa taarifa katika vikao mbalimbali, Halmashauri na shule wanawajibika kutoa matangazo kuhusu fedha zinazopokelewa, na matumizi yake katika mbao za matangazo za Halmashauri, shule, na sehemu za mikusanyiko ya wananchi. Lazima sasa kila mwananchi ajue ni kiasi gani cha fedha kimepokelewa katika Halmashauri au shule yake na jinsi zilivyotumika.... Huu ndio uwazi, uwajibikaji na ushiriki tunaoutaka."

Kila mmoja katika jamii anatakiwa kujisikia ni 'mmiliki' wa kamati, na kwamba anaweza kwenda na kuuliza maswali, kusuluhisha matatizo, kutoa mawazo na kupata taarifa. Kisheria kamati ya shule inawajibika kwa Mkurugenzi wa Halmashauri kwa matumizi mazuri ya fedha. Mwalimu mkuu pia anawajibika kwa kamati ya shule.

Uwezo wa kamati ya shule utaboreshwaje?

MMEM ina vipengele vingi vipya. Kimoja ambacho ni muhimu ni kwamba rasilimali nyingi sasa zinatumwa kwa kamati ya shule kwa ajili ya kuboresha elimu. MMEM inatambua umuhimu wa kuziwezesha kamati za shule kutekeleza majukumu yake kwa usahihi.

Kama hatua ya kwanza, MMEM inaeleza kuwa uelewa unatakiwa kujengwa kwa wadau muhimu wote, ikiwa ni pamoja na kamati za shule na jamii, kwa watu kuelewa malengo ya MMEM na majukumu ya kila ngazi. Hii itafanyika kwa kubadilishana taarifa, katika programu ya elimu na mawasiliano (IEC) katika utekelezaji wa MMEM kwa kipindi cha 2002 hadi 2006.

Pili, programu ya uwezeshaji itazingatiwa. Ngazi zote ni muhimu, lakini msisitizo zaidi unawekwa katika kamati ya shule. Mwongozo wa MMEM unafafanua kuwa dola za Marekani 500 (ambazo ni takribani shilingi za Tanzania 500,000) zitatolewa kwa uwezeshaji wa kamati za shule kwa kila shule na kila mwaka. Mafunzo yatafanywa na timu ya wilaya ambayo itafanya kazi na mashirika yasiyo ya kiserikali ili kufundisha wajumbe wa kamati za shule, timu ya uongozi wa shule na baraza la wanafunzi.

Nitafuatiliaje?

Kila mtu ana haki ya kupata taarifa, na kila mmoja ana haki ya kujua kuhusu utawala katika MMEM. Na kwa kuwa sasa unafahamu MMEM inasema nini kuhusu Kamati za shule, unaweza kuona ni jinsi gani Kamati hizo zinafanya kazi katika jamii yako na kutoa mawazo yakinifu yatakayosaidia kufanya mambo yawe bora zaidi. Kwa mfano unaweza kuuliza kama kamati ya shule yako inafanya vikao mara kwa mara na ni jinsi gani maamuzi yanachangiwa na kila mmoja katika jamii. Una haki ya kuuliza maswali na kupata majibu fasaha. Kwa mujibu wa mabadiliko ya Serikali, haikubaliki tena kwa kiongozi kutoa amri tu bila kuwasikiliza watu. Ni dhahiri mabadiliko huchukua muda, na hatutegemei kwamba kila kitu kitakuwa timilifu mara moja. Hata hivyo, una haki ya kuona maendeleo yakitokea.

Unaweza kupata habari kutoka kwa mwalimu mkuu, Afisa Elimu wa Wilaya, Diwani au Mbunge wako. Unaweza kuomba taarifa kutoka Mkutano wa Kijiji/Mtaa au vikao vya Halmashauri. Unaweza pia kuuliza Asasi Zisizo za Serikali (AZISE) katika eneo lako.



hakielimu

SLP 79401 • Dar es Salaam • Tanzania • Simu (022) 2151852 / 3 • Faksi (022) 2152449 • info@ hakielimu.org • www.hakielimu.org0